

CHANGAMOTO ZA KITEKNOHAMA KATIKA UFUNDISHAJI WA RIWAYA YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA

¹A. O. Owino, ²I. Simala na ³S. Choge .

¹Chuo Kikuu Kishiriki cha Kibabii

²Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

³Chuo Kikuu Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Ikisiri

Utafiti huu ulinua kutathmini changamoto za TEKNOHAMA katika ufundishaji wa Riwaya ya Kiswahili katika shule za upili Wilayani Kisumu Magharibi. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza iwapo TEKNOHAMA hutumiwa katika ufundishaji wa Riwaya ya Kiswahili katika shule za upili na kueleza changamoto za TEKNOHAMA katika ufundishaji wa Riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu uliongozwa na Mkabala wa Uhakiki Makinifu wa Mtalaa ambao hutumia mwelekeo wa nyanja mbalimbali na kuseta matumizi ya teknolojia kwa kutumia tarakilishi katika ufundishaji na ujifunzaji madhubuti. Sampuli lengwa ya utafiti huu ilishirikisha walimu wote wa Kiswahili wilayani Kisumu Magharibi waliopewa mafunzo na kuhitimu. Mtafiti aliwatumia walimu kutoka shule 23 za upili za umma Wilayani Kisumu Magharibi walioteuliwa kwa kuzingatia uteuzi wa kinasibu na utabakishaji. Utafiti huu ulitumia muundo wa usoroveya-elezi katika uchunguzi wa nyanjani. Uchunzaji darasani, usaili na hojaji zilitumika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa. Data zilichanganuliwa kwa kutumia Programu ya Tarakilishi ya Takwimu (SPSS). Kutokana na data, iligunduliwa kwamba walimu wengi hawakutumia aina mbalimbali za TEKNOHAMA kufundishia riwaya ya Kiswahili hata zilipopatikana. Aidha, utafiti huu ulifichua kwamba matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji wa riwaya yanakabiliwa na changamoto anuwai; ukosefu wa fedha, matumizi ya TEKNOHAMA kwa shughuli zisizowiana na ufundishaji na ukosefu wa miundo-misingi inayohitajika kuimarisha matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji wa riwaya ya Kiswahili. Kutokana na ugunduzi huu, utafiti huu umependekeza vyo vikuu vidurusu kozi ya mbinu za kufundishia ili kuhusisha matumizi ya TEKNOHAMA kwa ajili ya kuboresha ufundishaji wa walimu wanaofuzu kutoka vyo hivi. Utafiti huu pia umependekeza kwamba wizara ya elimu iandae semina, warsha na makongamano ili kuhimiza matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji pamoja na kulitengea somo la Kiswahili vipindi zaidi vya kufundishia riwaya ya Kiswahili kwa kuseta TEKNOHAMA katika ufundishaji. Aidha utafiti huu umewapendekeza walimu, wataalamu, watafiti na wachapishaji kuzingatia TEKNOHAMA katika shughuli zao kwa minajili ya kuboresha mchakato wa ufundishaji wa riwaya ya Kiswahili.